**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA

**Unapojibu tafadhali taja:**
Kumb. Na.HW/W:20/70/20

22/08/202

## TANGAZO KWA WATUMISHI WOTE.

Serikali kupitia sera yake ya kuboresha maisha ya watumishi wake imeamua kutoa mikopo kwa watumishi wa serikali za Mitaa kwa ajili ya ununuzi wa Magari, Samani, matengenezo ya Magari na Pikipiki. Serikali imetoa kiasi cha Tshs. 250,000,000/= kwa ajili ya mkopo huo.

Kwa tangazo hili Watumishi wote mnakaribishwa kutuma maombi kwa ajili ya mkopo tajwa hapo juu kwa masharti yafuatayo:

- Mkopo utatolewa kwa mtumishi mwenye Ajira ya Masharti ya Kudumu.
- Mkopo utatolewa kwa Mtumishi aliyethibitishwa kazini.
- Mkopaji anatakiwa kubakiwa na 1/3 ya mshahara wake baada ya makato ambayo yatarejeshwa kwa kipindi kisichozidi miezi 72 (miaka 6).
- Barua ya maombi iambatishwe na nakala ya Barua ya Ajira, Barua ya kuthibitishwa kazini, na hati ya Mshahara ya mwisho.
- Mkopo huu haununui deni kutoka taasisi nyingine za fedha.
- Mkopaji atalipa "Service charge" 3% na Protect fund 1% kutoka kwenye mkopo atakaokopa.
- Mkopo unaotolewa kwa mtumishi hauna riba
- Mkopo utatolewa kwa mtumishi mwenye mwenendo mzuri kazini na utendaji mzuri wa kazi katika Utumishi wa Umma.
- Mkopo huu hautatolewa kwa mtumishi aliyekwisha nufaika **(ana marejesho ya mkopo wa Serikali kwenye Salary Slip yake).**
- Fomu za maombi zinapatikana ofisi za Masjala ya Mkurugenzi Mtendaji (W) pamoja na kwenye website ya Halmashauri (www.bundadc.go.tz)
- Mwisho wa kupokea maombi ya mkopo huu ni tarehe 05/09/2022.
- Mkopaji anatakiwa kutuma barua ya maombi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, S.L.P 126, BUNDA, kupitia kwa Mkuu wake wa Idara na Mkuu wake wa Kituo cha Kazi.

## VIWANGO VYA MIKOPO VIPO KAMA IFUATAVYO:-

| **Aina ya Mkopo** | **Ngazi ya Mshahara** | **Kiwango cha juu cha mkopo** | **Muda wa Marejesho** |
|---|---|---|---|
| Mkopo Taslimu kwa ajili ya Ununuzi wa magari, pikipiki,samani na matengenezo ya vyombo vya usafiri | TGS A-C<br>TGTS A-C<br>TGHS A-C<br>TGOS A-C<br>TGHOS A-C | Milioni 15,000,000/= | Miezi 72 (Miaka 6) |
| | TGS D-F<br>TGTS D-F<br>TGHS D-F | Milioni 30,000,000/= | Miezi 72 (Miaka 6) |
| | TGS G-H<br>TGTS G-H<br>TGHS G-H | Milioni 40,000,000/= | Miezi 72 (Miaka 6) |
| | LSSE 1-4<br>TGTS I<br>TGHS I-J | Milioni 50,000,000/= | Miezi 72 (Miaka 6) |

Changwa M. Mkwazu
Mkurugenzi Mtendaji (W)
**BUNDA**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BUNDA